ENDELEZA NA HUISHA
UZIMA WA ULIMWENGU

# MSITU WA USHIRIKA

## KUHUISHA UZIMA WA ULIMWENGU NDANI YA USHIRIKA WA ANGLIKANA

Msitu wa Ushirika ni mpango wa *kimataifa* unaojumuisha shughuli za *jamii ya ndani* za uhifadhi wa misitu, upandaji wa miti na urejeshi wa mfumo wa ikolojia, zinazofanywa na majimbo, dayosisi na kanisa moja moja zilizopo ndani ya Ushirika wa Anglikana, ili kuulinda ulimwengu.



# Kuotesha ni kutumai

**Tunaishi katika wakati uliojaa majanga mengi ya kimataifa, yanayotokana na mlipuko wa Uviko-19, mabadiliko ya tabianchi, migogoro na majanga ya uhaba wa chakula. Katika hali yetu ya maumivu ya pamoja, tunahitaji kuona alama na vitendo vya matumaini.**

Msitu wa Ushirika ni alama na tendo la matumaini – jambo tunaloweza kulifanya kwa pamoja kama Kanisa la Mungu kwa ajili ya Ulimwengu wa Mungu, kadri tutakavyosonga mbele katika safari yetu baada ya Mkutano wa Lambeth.


Msitu wa Ushirika utachukua miundo mingi tofauti ndani ya Ushirika wa Anglikana, hivyo kuakisi wingi mkubwa wa chombo chetu cha kimataifa. Ninakuhimiza kujiunga kwenye mpango huu wa kusisimua, kwa njia yako mwenyewe, iwe ni kuhifadhi mazingira yenye thamani, kurejesha uzuri wa mazingira yaliyoharibiwa ama kuotesha jambo jingine jipya kabisa. Shughuli zote hizi hugusa vitendo vya kiroho pia, kwani:

- Kuotesha ni kutumai.
- Kuhifadhi ni kupenda.
- Kurejesha ni kuponya – kushiriki katika kazi ya upatanisho ya Mungu katika uumbaji wote.

Yesu mwenyewe mara nyingi ametajwa kuwa kwenye mazingira ya nje katika simulizi za injili. Matukio muhimu katika maisha yake duniani yalitokea akiwa milimani, Bahari ya Galilaya, jangwani na kwenye Mto Yordani. Katika usiku wa kuamkia kifo chake, Yesu, alijipatia amani akiwa katika kuomba kwa babaye katikati ya miti ndani ya Bustani ya Gethsemane.

Tafadhali ungana nasi katika kitendo hichi cha matumaini, upendo na uponyaji.

**Justin Welby, Askofu Mkuu wa Canterbury**



# Karibu kwenye Msitu wa Ushirika

**Msitu wa Ushirika ni mpango wa Ushirika wa Anglikana katika kuungana kwa pamoja kulinda na kurejesha misitu na mazingira mengine yaliyopo kote ulimwenguni. Kazi hii huakisi Alama ya Tano ya Dhamira ya Kanisa la Anglikana: *Kujitihadi kulinda asili ya uumbaji na kuendeleza na kuhuisha uzima wa ulimwengu.***

Msitu wa Ushirika ni mwitikio wa kiutendaji, kiroho na kiwakilishi, kufuatia majanga ya kimazingira, na ni kitendo cha kuonyesha matumaini ya Kikristo katika ustawi wa binadamu na uumbaji wote wa Mungu.

Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa bioanuai, kiwango kikubwa cha mateso yawapatayo binadamu, pamoja na kiasi kikubwa cha hali ya ukosenefu wa usawa, hatuna budi kuchukua hatua upesi na kwa ari ya kiwango cha juu.

Misitu husaidia kutengamisha hali ya hewa, kutulinda dhidi ya mafuriko, kuchuja hewa ya kaboni, huendeleza bioanuai na kutengeneza chakula na riziki kwa ajili ya jamii zilizopo kote ulimwenguni.

Tunakukaribisha kujiunga na mpango huu wa Msitu wa Ushirika. Kwa pamoja tunaweza kujifunza kutoka kwa kila mmoja wetu, kuhamasishwa na mipango ambayo teyari inafanya kazi na kusaidia kuwezesha makanisa katika uhifadhi, urejeshi na ufanyaji upya wa mazingira.

Dira iliyopo hapa ni mpango huu uweze kusukwa ndani ya maisha ya kiroho na ya kidini ya Kanisa, hivyo kuwasaidia watu kuunganisha imani zao na utunzaji wa uumbaji wa Mungu.



# Tengeneza urithi wa Mkutano wa kumi na tano wa Lambeth

**Ikiwa imezinduliwa katika Kasri ya Lambeth, kwenye Mkutano wa Lambeth wa mwaka 2022, Msitu wa Ushirika umelengwa kuwa miongoni mwa urithi wa Mkutano wa kumi na tano wa Lambeth – jambo lidumulo litakalowakilisha kiuhalisia azimio letu la pamoja kwa Alama ya Tano ya Dhamira ya Anglikana.**

Maaskofu wote pamoja na wenza wao wanaalikwa kushiriki katika mpango huu uhusishao Ushirika mzima, kisha kuushirikisha na dayosisi na jamii zao zilizopo kote ulimwenguni.

Msitu wa Ushirika umedhamiriwa kuwa dhima ya mkutano wa 2022 itakayosambazwa kwa wengine na itakayodumu kwa muda mrefu *"Kanisa la Mungu kwa ajili ya Watu wa Mungu – kutembea, kusikiliza na kushuhudia kwa pamoja."*



# Ukuzi wa Msitu wa Ushirika

## Jiunge na hatua ya matumaini ya kimataifa

Msitu wa Ushirika unaweza kuhusisha wigo mpana wa shughuli za utunzaji wa uumbaji. Popote ulipo duniani, unaalikwa kuanza mpango mpya wa kuutunza uumbaji – ama kuendeleza mpango uliopo teyari.

Kwa pamoja, miradi hii itaunda “msitu” pepe wa kimataifa. Baada ya muda, haya yote yataweza kudhihirishwa kupitia ushirikishaji wa mipango katika tovuti ya Msitu wa Ushirika

Shughuli za uhifadhi wa misitu zinaweza kuratibiwa kwenye jamii (na majimbo, dayosisi na sharika moja moja) ili ziweze kuendana na jeografia, tamaduni na mazingira husika.

Hivyo basi, “msitu” wa eneo fulani utakuwa wa tofauti kabisa na ule wa eneo lingine ndani ya Ushirika. Ujizatiti wa jamii fulani unaweza kujikita katika miti, lakini vilevile unaweza pia kuhusisha mbuga za nyasi, mabwawa au mazingira ya kingo za bahari.

*“Huu ni wakati wa kufanya uamuzi kuhusiana na ulimwengu, kiwango cha joto katika sayari kinaongezeka, bioanuai muhimu inayohifadhi na kuunganisha maisha kwenye sayari hii inaporomoka, na hatari ya anguko za kiuchumi kwa mamilioni ya watu inaongezeka. Changamoto hizi zina uhusiano, na misitu inaweza kutoa suluhisho muhimu la kiasilia ili kusaidia kutatua changamoto hizi tatu. Misitu si suluhisho pekee, hata hivyo, hatutaweza kufanikiwa bila hii.”*

*Muongozo wa Miti Trilioni katika kuwekeza kwenye urejeshi wa misitu*



# Ukuzi wa Msitu wa Ushirika

## Hatua zinazoweza kuchukuliwa na Maaskofu

Maaskofu wana wajibu muhimu katika kuhakikisha kuwa utunzwaji wa uumbaji unakuwa sehemu kuu ya dhamira, maisha na ushuhuda wa Kanisa. Unaweza kuchagua:
– Kuchochea mpango wa Msitu wa Ushirika kwenye dayosisi yako.

- Kujumuisha upandaji miti kwenye hafla na huduma za sherehe, kwa mfano siku za kusheherekea kumbukumbu ya kuzaliwa, ndoa, kuzaliwa kwa watoto, ubatizo na vipaimara. Kwa mfano, wapatie wanafunzi wa kipaimara mbegu au miche ya kuotesha na kuitunza kama ishara ya ukuaji wao kiroho.
- Tumia sauti na ushawishi wako kulinda na kurejesha misitu na asili nyingine za mazingira.
- Tenga eneo la ardhi kwa ajili ya kuotesha mbegu stahiki za miti ya kiasili ili dayosisi na jamii husika iweze kuwa na chanzo cha kupata miche ya miti ya asili kwa gharama nafuu.
- Shirikiana na vijana. Mara nyingi, hawa huathiriwa sana na mabadiliko makali ya tabianchi, na teyari wako katika kuchukua hatua. Watie moyo, paza sauti zao, wajumuishe kwenye mipango ya Msitu wa Ushirika na wasaidie kuunganisha harakati zao za kimazingira na imani yao.
- Tumia Msimu wa Uumbaji kama kipindi muhimu cha kuhamasisha mpango huu na utunzwaji wa uumbaji.

## Hatua zinazoweza kuchukuliwa na makanisa

Kwa kushirikiana kwa pamoja kama Ushirika wa Anglikana ulimwenguni kote, tunaweza kuacha alama kubwa katika mwitikio wa kimataifa wa utunzaji wa sayari yetu.

Kila hatua inayochukuliwa inaweza kusaidia kulinda mazingira na bioanuai; kutengeneza chakula ama eneo la uoto wa kijani kwa ajili ya watu kufurahia; kudhibiti mimomonyoko ya udongo na sehemu za fukwe; kupunguza hewa ya kaboni; kuzuia uharibifu wa mazingira; kupunguza uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo ya mijini; kuchangia katika kutunza amani.

Mradi si lazima uwe mpya – ila unaweza kuendeleza ama kuongeza shughuli fulani yenye manufaa kwa mazingira.

Unaweza kuchagua kufanya mradi unaohusisha:

- **Uhifadhi**: Tetea na chukua hatua ya kukomesha ukataji miti ama zuia uharibifu wa mazingira mengine.
- **Urejeshi**: Rejesha upya wa eneo fulani la ardhi iliyotelekezwa kwa uchafu ama mazingira mengine yaliyoharibiwa.
- **Uumbaji**: Anzisha mpango wa msitu kwenye ardhi ya kanisa ama unga mkono mradi unaohusiana na jambo hilo unaofanyika kwenye jamii pana zaidi.
- **Ukuzi**: Uhifadhi na urejeshi hauna budi kuzingatiwa kabla ya kuanzisha kitu kipya. Jambo jipya linapofanyika, mkazo unatakiwa uwekwe katika namna ya kukuza jambo hilo, na si tu katika kuanzisha. Ni vema aina ya mti sahihi ukapandwa eneo sahihi.
- **Kuzidisha**: Wasaidie wengine washiriki. Kuwa 'mzidishaji', kwa kutengeneza bustani ya miche ili kuwawezesha wengine kushiriki katika upandaji miti.







*"Katika suala la mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira na upotevu wa bioanuai, wengi wetu tumejifunza kuitikia haya kwa kujaa fadhaa, tunaona dunia inapoelekea na tunainua mikono yetu juu. Ndio, ni hali mbaya, lakini ni ngumu sana na kubwa sana na inatulemea sana. Hakuna chochote tunachoweza kufanya kuizuia. Mwitikio wa namna hii si tu kwamba si wa kweli, lakini pia, kimsingi haujiwajibishi. Tambua kwamba una bahati kubwa ya kuwa hai katika kipindi ambacho unaweza kuweka tofauti inayoweza kugeuza mustakabali wa maisha yetu sote hapa duniani. Haujaishiwa nguvu. Kila moja ya hatua zako ina maana kubwa na u sehemu ya mlango mkubwa wa mafanikio ya binadamu kwenye historia"*

**Christiana Figueres "Mustakabali Tunaouchagua"**

*Ni wakati wa kuchagua kati ya uzima na mauti.*

**(Kumbukumbu la Torati 30:19)**

# Msitu wa Ushirika – Tafakari ya Kibiblia

*"Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo, katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi."*

***"Na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa."***
*Ufunuo wa Yohana 22:1-2*

Katika kukabiliana na janga linaloendelea la Uviko-19 na madhara yake makubwa... katikati ya masaibu matatu ya kimazingira ya mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa bioanuai na uchafuzi wa mazingira... na uhasama na migogoro inayoendelea kushika kasi kwenye ulimwengu huu, maneno haya kutoka kwenye kitabu cha Ufunuo yanatukumbusha juu ya madhumuni ya Mungu ya ukombozi. Moyo wa Mungu umeazimia "kuwaponya mataifa".

Katika maono ya Ufunuo huu, miti ya uzima imesimama upande huu na upande huu wa mto wa maji ung'aao kama bilauri, utiririshao maji ya uzima. Miti hii hutoa chakula na majani yake huleta uponyaji. Ni mandhari ya wingi, urejeshi na uzima.

Simulizi ya Biblia inaanza na bustani ya miti, ambayo binadamu anaagizwa "kuilima na kuitunza" (Mwanzo 2:15), na inafikia tamati katika mto uliozungukwa na miti. Maono yaliyopo kwenye kitabu cha Ufunuo si urejelezi wa hali ya awali ya Uumbaji. Badala yake, jambo jipya linatambulishwa kwenye bustani takatifu – mji uliorejeshwa na ulio mtakatifu. Ujumbe mahiri ulioje kuhusu uwezekano wa kugeuzwa kwa tamaduni za binadamu na mifumo ya miji!

Throughout the Bible, trees are frequently part of the story as people encounter God. Abraham entertained angels at the oaks of Mamre. Moses stood shoeless next to the burning bush. Elijah sat in despair by a broom tree and was given refreshment. Nathaniel was called from under a fig tree to a new way of living, and Zacchaeus climbed the sycamore tree because he was desperate to see Jesus pass by.

epls. Pink para not included in translation.

Yesu mwenyewe aliifahamu miti. Kutoka kwenye hori ambapo walimlaza mtoto aliyezaliwa, hadi katika kazi zake kama fundi seremala, na katika msalaba alipofia, mti uligusa sehemu kubwa ya maisha yake. Yesu alipata utulivu kwenye mazingira ya asili, hapo alizungumza na Baba na alitumia jioni yake ya mwisho kwenye Bustani ya Gethsemane katika Mlima wa Mizeituni.

Watu hudai kuhisi kuunganishwa na muumbaji wao wakiwapo kwenye mazingira ya asili. Kutembea katikati ya mazingira ya msitu kumeonekana kuunufaisha mwili, akili na roho. Watu wengi, wakiwa kwenye mandhari za asili, hujihisi kwamba wanaweza kujiunganisha katika kuuimba wimbo wa uumbaji ambao huusikia pande zote zinazowazunguka.: "Kila mwenye pumzi na amsifu Bwana!" (Zaburi 150:6)

Hata hivyo, misitu na jamii nyingine za mimea zimewekwa hatarini, pamoja na kiwango kikubwa cha spishi mbalimbali zinazotegemea mimea hiyo, ikiwa ni pamoja na binadamu.

Tuko katika janga la tabianchi na la kiikolojia. Tuko katika wakati wa kufanya maamuzi kwa ajili ya mustakabali wa ubinadamu na maskani yetu tuliyoizoea, dunia.



*“Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuna hatua chache zilizo muhimu, zipasazwo kufanyika upesi, au zilizo rahisi tu, kama vile upandaji wa miti. Teknolojia hii ya kale ya uchujaji wa hewa ya kaboni haihitaji teknolojia ya kiwango cha juu, ni salama kabisa na ya gharama nafuu sana. Kiuhalisia, inageuza mchakato uliopelekea mabadiliko ya tabianchi, kwani miti (pamoja na mkusanyiko wa viumbe hai vingine) hukua, hufyonza Kaboni Dioksidi ($CO_2$) kutoka kwenye hewa, huachilia hewa ya oksijeni na kuirudisha kaboni mahala pake sahihi: kwenye udongo. Pia, miti huunda mandhari za kupendeza ndani ya miji, hushusha halijoto, huweza kuzalisha chakula, na kustawisha chemichemi za maji vijijini na kwenye maeneo ya vitongoji vya miji.”*

**Mustakabali Tunaouchagua, Christiana Figueres na Tom Rivett-Carnac, p133.**

# Kwanini Msitu wa Ushirika ni muhimu?

## Kushughulikia Janga la Kimazingira

The integrity of creation is under threat and at risk of collapse. The life systems of the earth are under severe strain from the triple environmental crises of climate change, biodiversity loss and pollution.

**epls.** Pink para not included in translation.

*“Binadamu hupigana vita na mazingira asilia. Jambo hili ni upuuzi na muundo wa kujiuwa wenyewe. Matokeo ya uzembe wetu teyari yamejidhihirisha katika taabu azipatazo binadamu, zizidisho hasara za kiuchumi na kukuza mporomoko wa maisha Duniani.”*[1]
Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres

Majanga ya kimazingira ni tishio kubwa kwa mamilioni ya watu na spishi za mimea na wanyama kote ulimwenguni. Maafa yanayojiinua taratibu, kama vile ukame na ongezeko la kina cha bahari, pamoja na maafa yajiinuayo kwa ghafla, kama vile majanga ya mafuriko na kuungua kwa misitu, husababisha vifo, huharibu makazi na nyumba zetu pendwa, huondosha riziki, husababisha ukosekano wa chakula, hulazimisha watu kuhama, huvuruga jamii na kutapanya familia. Athari za majanga haya ni kubwa, katika nyanja ya kiuchumi na katika maumivu yasababishwayo nayo, ambayo kwa kiwango kikubwa huwakumba vijana.

1 The United Nations Environment Programme synthesis report Making Peace With Nature opens with these stark words from the UN Secretary General.

**epls.** Footnote not included in translation.

## Kuishi Alama ya Tano ya Dhamira Yetu

Waanglikana kwa muda mrefu wameambatana na uelewa mkamilifu wa dhamira, ambayo si tu huchukulia kwa uzito suala la utunzwaji wa uumbaji, bali huona pia jambo hilo kuwa moja ya njia kuu tunazoshuhudia kwa pamoja simulizi endelevu ya upendo wa Mungu ulimwenguni.

Hili limeelezwa kinagaubaga katika Alama ya Tano ya Dhamira ya Anglikana: ***Kujitahidi kuulinda unyofu wa uumbaji, na kuendeleza na kuhuisha uzima wa ulimwengu.***

Msitu wa Ushirika ni njia ya kimatendo ya:

- Kuulinda unyofu wa uumbaji, na kuendeleza na kuhuisha uzima wa ulimwengu.
- Kusaidia katika upandaji miti na uhifadhi wa bioanuai, kuwezesha makazi, kulinda mifumo ya ikolojia na kuondoa baadhi ya kaboni dioksidi kutoka kwenye angahewa.
- Kutambua uhusiano na utegemezi uliopo baina ya maisha yote yaliyopo duniani.

Kufanya kazi kulinda na kurejesha misitu ni mojawapo tu ya hatua nyingi muhimu zinazohitajika kufanywa ili kukabiliana na janga la kimazingira. Msitu wa Ushirika unatumainiwa kuwa kama lango la suala na hatua kubwa zaidi ya kimazingira, iwahabarishayo na kuwahamasisha Waanglikana waliopo kila mahali kufanya utunzaji wa mazingira kuwa sehemu muhimu ya ufuasi wao.

Msitu wa Ushirika una thamani ya kiuwakilishi pia.

- Upendo na hali yetu ya kuujali uumbaji wa Mungu, maskani yetu sote
- Ufuasi wetu wa Kikristo
- Wajibu wetu kwa Alama za Dhamira ya Anglikana
- Ujihusishaji wetu kwa upana katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi, kuhifadhi bioanuai na kupunguza uchafuzi wa mazingira

Hivyo, Msitu wa Ushirika unaweza kuwa chanzo ya hamasa, inayowakilisha maadili yetu ya pamoja.

Msitu wa Ushirika pia ni kitendo kinachoonyesha tumaini la Ukristo. Katikati ya kukabiliana na janga linaloendelea la Uviko-19 pamoja na majanga ya kimazingira, uundwaji wa Msitu wa Ushirika ni chaguzi la kutengeneza siku njema zaidi za baadae, *kwa pamoja*.



# Kuchangia katika Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa

Ukiwa unawakilisha mamilioni ya Wakristo na ukiwa ndani ya nchi 165, Ushirika wa Anglikana una mchango muhimu katika kuunga mkono Malengo ya kimataifa ya Maendeleo Endelevu, yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa.

Kila hatua tunayochukua huongezeka juu ya nyingine. Kwa kuanzisha Msitu wa Ushirika, tunaweza kuchangia katika Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu: **Lengo 1** Kumaliza umaskini, **Lengo 2** Kumaliza njaa, **Lengo 3** Afya nzuri, **Lengo 6** maji, **Lengo 11** jamii endelevu, **Lengo 13** hatua za kukabiliana na tabianchi, **Lengo 15** maisha ardhini, **Lengo 17** ushirikiano.
















# Usaidizi na Rasilimali

## Jiunge na Jamii ya Msitu wa Ushirika

Katika mwaka wa kwanza wa maisha ya Msitu wa Ushirika, mtu wa maliasili ataajiriwa kwa masaa fulani kwa siku kutoa msaada kwa dayosisi, kushirikiana na wadau katika kupata msaada wa kiufundi, kusaidia katika kupata ufadhili wa kiuwekezaji kwa ajili ya dayosisi, kufuatilia maendeleo, na kuratibu mawasiliano, yanayojumuisha ushirikishaji wa simulizi na matukio.


Msitu wa Ushirika si mradi utakaofadhiliwa, kusimamiwa au kuundwa na chombo fulani kutoka nje.

Endelea kuwasiliana na timu hii kupitia: **communion.forest@aco.org**

Taarifa zaidi zinapatikana kwenye tovuti ya Msitu wa Ushirika na kwenye kifurushi cha rasilimali cha Msitu wa Ushirika.

Jiunge nasi mtandaoni, ili tushirikishane simulizi zetu kuhusu maisha ya Msitu wa Ushirika wa Lambeth katika kipindi cha miaka kumi ijao.

Nyenzo zinapatikana katika lugha rasmi nne za Ushirika: Kihispania, Kireno, Kifaransa na Kiingereza.



## Usomaji Zaidi

Kuna rasilimali nyingi nzuri sana zinazopatikana kutoka kwa taasisi za kitaalamu, zitakazokusaidia kufanya maamuzi na kupanga mipango vyema:

Zana ya utathmini wa mradi wa Miti Trilioni: Hutoa eneo zuri sana la kuanzia katika kutafakari uhifadhi, urejeshi wa misitu na upandaji wa miti. Zana hii hutoa muongozo angavu, unaotekelezeka, uonyeshao vigezo vipelekeavyo urejeshi mzuri wa msitu, na kukuwezesha kuutathmini mradi ulioupanga dhidi ya vigezo hivyo. Pia tizama mradi wa Miti Trilioni ili kupata maarifa ya namna mipango ya ndani ya jamii inaweza kukua na hata kufikia harakati ya kimataifa.

Tembelea ‘Interfaith Rainforest Initiative’ (IRI) na ‘Faith for Forests’ kupata taarifa juu ya umuhimu wa kulinda misitu ya mvua ya tropiki – na wajibu wa viongozi wa dini katika hilo. IRI ina rasilimali nyingi muhimu, zinazojumuisha seti ya zana za imani na miongozo ya rasilimali.

IRI pia imechapisha kijitabu muhimu sana kwa ajili ya viongozi wa dini na jamii za imani, kihusucho uhifadhi wa misitu, kwa ajili ya kutumiwa ndani ya kipindi cha Mwongo wa Umoja wa Mataifa wa Urejeshi wa Mfumo wa Ikolojia.

Muungano wa Kimataifa kwa ajili ya Uhifadhi wa Mazingira Asilia (IUCN) umezalisha seti nzuri sana ya Zana za Uratibu wa Jamii katika Urejeshi wa Mfumo wa Ikolojia “ili kuwatayarisha, waleta-mabadiliko, kwa kuwapatia nyenzo, maarifa, na rasilimali zinazohitajika kurejesha mifumo ya ikolojia katika hali yake ya awali iliyosheheni uzalishaji, na maeneo yenye ustawi.” Hujumuisha mashamba, misitu, vyanzo vya maji yasiyo na chumvi, mbuga za nyasi, vichaka na maeneo ya miti michache, milima, bahari na fukwe, pamoja na maeneo ya miji.

Kanuni za Uoteshaji Miti wenye Mafanikio, muongozo mfupi kutoka kwa Kituo cha Utafiti wa Kimataifa wa Misitu (CIFOR) uhusuo uanzishwaji wa mradi wa upandaji miti. Huu umeweka msingi imara kwa ajili ya mpango wowote. Umeelezea kauli ya msingi inayopasa kutegemeza shughuli yoyote: mti sahihi kwa jili ya eneo sahihi na madhumuni sahihi. CIFOR ina taarifa zaidi na za kinagaubaga zaidi kwenye tovuti yake. Ikishirikiana na CIFOR, ni Jukwaa la Kimataifa la Mazingira, lililo jukwaa lenye maarifa mengi zaidi kuhusiana na mazingira endelevu.


Kupata mawazo na hamasa zaidi, tizama tafiti mbalimbali kutoka kwa Ushirika wa Anglikana, kupitia tovuti ya Msitu wa Ushirika.

The Communion Forest initiative has been developed by a working group of bishops from across the Communion, the Anglican Communion Environmental Network and the Anglican Alliance.

epls. Pink para not included in translation.

ANGLICAN COMMUNION ENVIRONMENTAL NETWORK

ANGLICAN ALLIANCE
Development · Relief · Advocacy



LAMBETH CONFERENCE

www.lambethconference.org
info@lambethconference.org

**Fuatilia mazungumzo yaliyopo**

www.facebook.com/LambethConference
www.twitter.com/LambethConf
#LambethConf

ANGLICAN COMMUNION
IN OVER 165 COUNTRIES

www.anglicancommunion.org
www.facebook.com/theanglicancommunion
@AnglicanWorld

FSC
www.fsc.org
MIX
Paper | Supporting responsible forestry
FSC® C005143

KISWAHILI

